

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA

**Kumb Na: AB.134/358/01/16**

**03 Januari, 2020**

### **TANGAZO LA KAZI**

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watazania wenye sifa na uwezo kujaza nafasi wazi mbili (2) kwa kazi ya Dereva kama zilivyobainishwa katika tangazo hili.

#### **1.0. DEREVA (2)**

##### **1.1. SIFA ZA MUOMBAJI.**

- I. Cheti cha Mtihani wa Kidato cha IV,
- II. Leseni ya daraja "C1" au "E" ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda wa mwaka mmoja bila kusababisha ajali,
- III. mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo cha Usafirishaji (NIT).
- IV. Waombaji wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

## **1.2. MAJUKUMU YA KAZI.**

- II. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- III. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- IV. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- V. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- VI. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- VII. Kufanya usafi wa gari, na
- VIII. Kufanya kazi nyingine kadri anavyoelekeza na Msimamizi wake.

## **2.0. MASHARTI YA JUMLA**

- I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania,
- II. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa,
- III. Waombaji wote wawe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45,
- IV. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- V. Maombi yote yaambatane na vyeti vya kidato cha nne, pamoja na vyeti vingine kama ilivyoanishwa katika sifa za kazi hapo juu.
- VI. Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA**
- VII. Picha moja “Passport size” ya hivi karibuni.
- VIII. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na Baraza la Mitihani Tanzania – (NECTA).

IX. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

**Maombi yote yatumwe kwa: -**

**MTENDAJI MKUU,  
WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA,  
S.L.P 724,  
DAR ES SALAAM.**

**Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 17 Januari,2020**

Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAKUBALIWA.**